



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



TANGAZO


MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA HALMASHAURI YA WALAYA YA NJOMBE KUHUSU KUFUNGULIWA RASMI KWA DIRISHA LA UTOAJI WA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI (10%) KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAYU.

HALMASHAURI IMETENGA JUMLA YA **SHILINGI 1,163,722,992.05** KWA AJILI YA UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI, MKURUGENZI MTENDAJI ANAWATANGAZIA WANAVIKUNDI WOTE WENYE SIFA KUTUMA MAOMBI YA MIKOPO KUPITIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA WEZESHA PORTAL. DIRISHA LA MAOMBI LIMEFUNGULIWA KUANZIA 01.10.2024 NA LITAFUNGWA TAREHE 30.10.2024.


Christopher A. Sanga

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA NJOMBE



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE



TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UWEPWA WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA WATU WENYE ULEMVU

(limetolewa kwa kuzingatia kanuni ya 8 (1))

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia wananchi wote uwepo wa fedha kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kiasi cha **shilingi 1,163,722,992.05** kimetengwa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kupeleka maombi katika Ofisi za kata zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotaka kuomba mkopo vinatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Wanakikundi wawe ni raia wa Tanzania wenye akili timamu na umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea isipokuwa kwa kundi la vijana mwisho miaka 45;

- (ii) Kikundi kiwe kimetambuliwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa mujibu wa mfumo wa utambuzi wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu;
 - (iii) Kikundi kiwe kinajishughulisha au kinakusudia kuanzisha ujasiriamali mdogo au wakati;
 - (iv) Kikundi kiwe na wanakikundi kuanzia watano isipokuwa kikundi cha watu wenye ulemavu ambacho kitakuwa na wanakikundi wasiopungua wawili (2);
 - (v) Kikundi kiwe na akaunti ya benki; na
 - (vi) Kikundi kisiwe na wajumbe wenye ajira rasmi;
 - (vii) Kikundi Kiwe kimepata mafunzo.
- Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatanisho vifuatavyo;- cheti cha usajili, barua ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji na kata, muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko la mradi unaombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani mfumo na taarifa ya akaunti benki.
- Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 30.10.2024
- Tangazo hili limetolewa na: -**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Njombe